

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**



*Dar es Salaam
02 Mei, 2026*

YAH: UTEUZI NA UHAMISHO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi na uhamisho wa viongozi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, uteuzi na uhamisho huo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mhe. Dkt. Evaline Wilbard Munisi (Mb.) ameteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano). Mhe. Dkt. Munisi anachukua nafasi ya Mhe. Rahma Riyadh Kisuo (Mb.) ambaye uteuzi wake umetenguliwa;
- (ii) Bw. Eliakim Chacha Maswi amehamishwa kutoka Wizara ya Katiba na Sheria kwenda kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; na
- (iii) Dkt. John Antony Jingu amehamishwa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwenda kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

